




JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA KISARAWÉ



TANGAZO LA ZABUNI

KIPINDI CHA 2022/2023

Date: 04/08/2022

1. LGA/009/HQ/2022/2023/N/01: KUTOA HUDUMA YA CHAKULA KATIKA HALMASHAURI YA WILAYA
2. LGA/009/HQ/2022/2023/N/02/1: KUSAFISHA MAZINGIRA YA OFISI ZA HALMASHAURI.
3. LGA/009/HQ/2022/2023/N/02/2: KUSAFISHA MAENEO YA NJE YA HOSPITALI YA WILAYA
4. LGA/009/HQ/2022/2023/N/02/3: KUFANYA USAFI WA NDANI KATIKA MAJENGO YA HOSPITALI YA WILAYA

1. Halmashauri ya Wilaya Kisarawe imetenga fedha kwa ajili ya kupata huduma ya tajwa hapo juu kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Huduma ya hizi zinatarajiwa kutolewa katika maeneo ya Halmashauri na Hospitali ya wilaya.
2. Halmashauri ya Wilaya Kisarawe inapenda kuwaalika watu binafsi, Makampuni, Mashirika, Taasisi au vikundi vya watu vilivyosajiliwa kisheria wenye nia, uwezo na uzoefu wa kufanya kazi hizo kutuma maombi yao kwa zabuni hizi.
3. Waombaji wanakaribishwa siku ya tarehe **09/08/2022** kwa ajili ya kutembelea maeneo ya kazi na kupata ufafanuzi wa yaliyomo katika nyaraka za zabuni. Kazi zote zipo katika eneo la Mamlaka ya mji mdogo wa Kisarawe.
4. Maombi yote ya zabuni yazingatie masharti yafuatayo:
  - i) Nyaraka za zabuni zitapatikana kwa malipo ya Shilingi mia moja elfu tu (100,000/=) kwa kila zabuni ambayo haitarudishwa.


- ii) Ombi la zabuni liwe na jina na anuani halisi ya mwombaji, aidha aonyeshe mahali ofisi zake zilipo au anapoweza kupatikana (Physical address)
- iii) Zingatia kuwa “form” ya maombi ya Zabuni inajazwa na kusainiwa na mwenye uhalali wa kisheria “Power of Attorney”.
5. Mwombaji aonyeshe vifaa alivyonavyo, idadi ya wafanyakazi na uzoefu wao.
6. Mwombaji awasilishe nakala halisi na nakala mbili zilizozalishwa, endapo maelezo ya nakala zilizozalishwa na Nakala halisi yatatofautiana nakala halisi ndio itatumika kwenye tathmini.
7. Zabuni ijazwe vizuri, iwekwe kwenye bahasha isiyo na maandishi yoyote na juu ya bahasha iandikwe, namba ya zabuni, jina la kazi inayoombwa, bahasha iandikwe kuwa ni Nakala halisi au nakala iliyozalishwa, kisha iandikwe anuani tajwa hapa chini:

**KATIBU BODI YA ZABUNI,  
HALMASHAURI YA WILAYA,  
S.L.P 28001,  
KISARAWAWE.**

Anwani hiyo ionekane juu ya bahasha bila kuwekwa alama yoyote.

8. Mwombaji awe na uzoefu wa miaka isiyopungua mitatu katika huduma husika na atoe maelezo jinsi gani atadumisha kazi ya husika.
9. Mwombaji atakayeshindwa masharti haya atakuwa amejiondoa mwenyewe kwenye mchakato mzima wa zabuni.
10. Uongozi haulazimiki kuchagua zabuni yoyote.
11. Zabuni zitawasilishwa kwa anwani tajwa hapo juu.  
Mwisho wa kupokea zabuni ni saa nne (4:00) kamili asubuhi (saa ya Afrika Mashariki) ya tarehe **11/08/2021** katika ofisi za Halmashauri ya Wilaya
12. Waombaji au wawakilishi wa waombaji wanaalikwa kushuhudia ufunguzi. Ufunguzi utafanywa mara tu baada ya saa ya mwisho ya kupokea zabuni mbele ya waombaji au wawakilishi wa waombaji waliowachagua kuhudhuria ufunguzi huo.
13. Zabuni ambazo zitachelewa kwa muda uliopangwa na zabuni zitakazotumwa kwa mtandao (e-mail) hazitapokelewa.
14. Anuani ya kutuma zabuni hii ni:

**KATIBU BODI YA ZABUNI,  
HALMASHAURI YA WILAYA,  
S.L.P 28001, KISARAWAWE.**

  
James C. Chitumbi

**KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI (W)  
KISARAWAWE**

